**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**
Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz

**OFISI YA MKUU WA MKOA**
**3 Barabara ya Rashidi Kawawa**,
S.L.P 5429,
**12880 -DAR ES SALAAM.**
**Tanzania**

**20.09.2018**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## RC MAKONDA AWAPA MIEZI MINNE WAAJIRI KUHAKIKISHA WANAWAAJIRI WATU WENYE ULEMAVU KAMA SHERIA INAVYOWATAKA.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo ametoa miezi minne kwa waajiri wa Makampuni na Mashirika kuhakikisha wanawaajiri watu wenye ulemavu Kama Sheria ya Walemavu ya 2010 na Mikataba ya kimataifa ya mwaka 2006 iliyoridhiwa na Tanzania mwaka 2009 sura ya 27 inavyowaaagiza kufanya hivyo.

RC Makonda amesema ifikapo Mwezi January mwakani ataanza ziara ya kutembelea kwenye kila Kampuni na Taasisi Jijini humo kukagua Kama wametekeleza Sheria na agizo hilo ambapo watakaobainika kukaidi watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Aidha RC Makonda amesema kitendo cha kuwaajiri walemavu kitapunguza ongezeko la ombaomba, ukatili, utupwaji wa watoto wenye ulemavu, kuhamasisha walemavu kusoma pamoja na kuwawezesha walemavu kuhudumia familia zao.

***"Hatuwezi kuwa na ndugu zetu wamesoma na wanasifa za kupata Kazi lakini tunawanyima matokeo yake wengine wanaishia kujinyonga, kinamama wanatupa Watoto wenye ulemavu, mila potovu zinaendelea kupoteza haki na mwisho wanabaki wakiwa Masikini na kushindwa hata kumudu gharama za Matibabu, Jambo hili sio la kufumbia macho"*** alisema RC Makonda

Kwa mujibu wa Sheria ya ajira kwa watu wenye ulemavu No. 9 ya mwaka 2010 kifungu cha 31 inamtaka kila mwajiri mwenye wafanyakazi zaidi ya 20 kuhakikisha 3% ya wafanyakazi ni watu wenye ulemavu.

**RAIS MAGUFULI AMEONYESHA DIRA KWA KUTOA KIPAUMBELE CHA AJIRA KWA WALEMAVU, NI WAKATI SASA KWA WAAJIRI KUTEKELEZA SHERIA.**

Imetolewa na:-


Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**